SIGNAL Publishers
Igniting thinking

# DARASA LA NANE

**SIGNAL 002**

# SIGNAL EXAMS 2020
# JARIBIO LA PILI

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA**
**KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na sio katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano**

    **Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Sehemu ya jikoni yenye bomba la maji la kuoshea vyombo huitwa
   A. chano
   B. upawa
   C. karo
   D. legeni

   Jibu sahihi ni C. (**karo**

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

**1** [A] [B] [C] [D]   **11** [A] [B] [▬] [D]   **21** [A] [B] [C] [D]   **31** [A] [B] [C] [D]   **41** [A] [B] [C] [D]

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa**

SIGNAL

*© Signal Publishers Limited 2020*

*Website: www. signalpublishers.com. Email. info@signalpublishers.com*

SignalPublishers   @SignalPublishers

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Mzazi yeyote hana budi ___1___ malezi ya mwanawe kwa njia ___2___. Sharti aelewe kuwa kuimarika kwa afya, yaani ___3___ yake kunahitaji ___4___ lishe bora. ___5___, ni vyema kuelewa ___6___ kuwa mtoto anahitaji kukuzwa kihisia. Akipatwa na maafa yoyote ___7___ hata yawe madogo kiasi gani, mzazi awe pale ___8___. Zaidi ya yote, matendo ya mzazi mwenyewe ___9___ kielelezo bora kwa mtoto huyu kwani ___10___.

1. A. kumwajibikia B. kuyawajibikia C. Kuiwajibikia D. kuwajibika
2. A. yafaayo B. yafaao C. ifaao D. ifaayo
3. A. rai B. nia C. ari D. mwili
4. A. akule B. alishe C. alishwe D. akulishwe
5. A. Hadi B. Bali C. Ama D. Aidha
6. A. kuzuri B. vizuri C. mzuri D. pazuri
7. A. , B. ; C. : D. __
8. A. kumfariji B. kumliza D. kumtukuza D. kumbeza
9. A. awe B. kiwe C. yawe D. yasiwe
10. A. uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi B. mwana akibebwa hutazama kisogo cha mamaye C. mwenye macho haambiwi tanzama D. ukiona vyaelea jua vimeundwa

Sitamsahau jirani yangu Bwana Mambo. ___11___ ustaarabu maishani. Ustaarabu ni ___12___. Jirani huyu hakuwa mwenye ___13___ ___14___ alijitolea ___15___ masomo yangu wavyele wangu walipokuwa hawana hali.

11. A. Ndio alionifunza B. Ndiwe aliyenifunza C. Ndio alinifunza D. Ndiye aliyenifunza
12. A. hali ya kuwahudumia wengine bila kuhitaji malipo
    B. tabia ya kuwa mchangamfu na mwenye furaha kwa watu
    C. hali ya kuwa na mienendo inayokubalika katika jamii
    D. kuwa na maisha yanayotamaniwa na wengine
13. A. mkono birika B. mkono mzito C. mkono wazi D. mkono mrefu
14. A. ila B. kwani C. wala D. ilhali
15. kuidhamini B. kuyathamini C. kuithamini D. kuyadhamini

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. Neno ng'onda lina sauti ngapi?
   A. Mbili
   B. Sita
   C. Saba
   D. Tano
17. **Andika wingi wa sentensi ifuatayo.**
   Jirani yangu amenunua cherehani.
   A. Majirani zetu wamenunua vyerehani.
   B. Majirani yetu wamenunua vyerehani.
   C. Jirani zetu wamenunua vyerehani.
   D. Majirani zangu wamenunua vyerehani.
18. Chagua orodha yenye maneno ya aina moja.
   A. Maji, madawati, uyoga.
   B. Wema, huzuni, amani.
   C. Kenya, taifa, wananchi.
   D. Bunda, kitita, manukato.
19. Mwenzako akifikwa na janga utamliwaza kwa kumwambia
   A. ashakum
   B. kunradhi
   C. pole
   D. simile.
20. Ni uambatanisho upi ulio sahihi?
   A. Mbuzi - Katama
   B. Nzige - Kiwavi
   C. Nzi - Buu
   D. Ngamia - Kivinimbi.
21. **Kanusha sentensi ifuatayo.**
   Mwanao akikuona atakukimbilia.
   A. Mwanao hatakuona wala kukimbilia.
   B. Mwanao asipokuona hatakukimbilia.
   C. Mwanao asipokuona hakukimbilii.
   D. Mwanao akikuona asingekukimbilia.
22. **Tegua kitendawili kifuatacho.**
   Likienda hulia likirudi halili.
   A. Debe
   B. Radi
   C. Jua
   D. Upepo.
23. **Ni sentensi ipi iliyo sahihi?**
   A. Mama alinipea pesa ya matumizi.
   B. Alipanguza meza kwa kitambaa kile.
   C. Mwalimu alitufunza mambo kadhaa wa kadhaa.
   D. Tuliutikisa mti matunda yakaanguka.
24. **Unganisha sentensi ifuatayo kwa usahihi.**
   Maua alipika wali. Wali ulikuwa kwa Hamisi.
   A. Wali ulipikwa kwa Hamisi na Maua
   B. Maua alipikiwa wali kwa Hamisi.
   C. Hamisi alipikiwa wali kwa Maua.
   D. Wali ulipikwa na Hamisi kwa Maua.
25. **Tambua maneno yaliyoangaziwa kwenye sentensi ifuatayo.**
   Vitabu **vizuri** vitanunuliwa **Alhamisi**.
   A. Kielezi, nomino
   B. Kivumishi, nomino
   C. Kivumishi, kielezi
   D. kielezi, kiwakilishi.
26. Ugonjwa uwashikao watoto na kuwafanya wakohoe sana na kutoa sauti kama ya filimbi ni
   A. waba
   B. kifaduro
   C. mafua
   D. kifuakikuu.
27. **Chagua sentensi iliyo katika hali timilifu.**
   A. Kijakazi alikuwa akipiga deki.
   B. Mtoto atalazwa kitandani.
   C. Najua tofauti ya mandhari na mandari.
   D. Jua limewaka sana msimu huu.
28. Mtu anayehamia katika nchi isiyo yake na kumiliki ardhi huko ni
   A. mkiritimba
   B. mlowezi
   C. mkimbizi
   D. mzalendo.
29. Kutokana na kitenzi **vumilia**, tunapata kivumishi kipi?
   A. Mvumilivu
   B. Kuvumulia
   C. Uvumilivu
   D. Mvumo.
30. **Si vyema mtu kujitaabisha sana akijaribu kutenda mambo yaliyo juu ya uwezo wake.**
   Chagua methali inayolingana na maelezo haya.
   A. Mtaka unda haneni.
   B. Mtu hujikuna ajipatapo.
   C. Penye nia pana njia.
   D. Mwanzo wa ngoma ni lele.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31- 40.***

Hapo zamani za kale, wanyama waliishi katika nchi moja iliyoshuhudia ustawi na furaha isiyo kifani. Kulikuwa na mvua na jua kila siku ya Mungu. Kwa hivyo, kuadimika kwa maji au majani ikawa ni ndoto tu. Wakaiita nchi yao Baraka. Katika maisha ya pepo kama haya, huwakuona haja ya kuwa na kiongozi.

Walipoendelea kuzaana na idadi yao kukithiri balaa ilizuka. Wanyama walioishi mwanzoni kwa buraha wakaanza kuishi kwa **rabsha**. Ambapo hapo zamani palikuwa na udugu sasa uliota uhasama. Vita vikawa ni vya mtindo mmoja; isiwe malishoni, visimani na hata kwenye rasilimali. Wanyama wengi wakakata kamba kwenye vurumai hiyo. Baada ya wazee kufanya kikao, mkutano mkubwa uliitishwa. Wakaja wanyama wengi. Wakongwe kwa vijana, wa kike kwa wa kiume. Mwenyekiti, ambaye alikuwa Nyani, aliongoza mkutano akiwa ananing'inia kwenye tawi la mti mkubwa ili wanyama waliokuwa pande zote wamwone na kumsikia. Iliafikiwa kuwa Baraka ilihitaji kiongozi na Simba akachaguliwa kutekeleza jukumu hilo.

Uongozi wa Simba ulianza vizuri, utawala ukiendeshwa kwa hekima, haki na kujali maslahi ya wanyama wote. Amani na ustawi vikarudi. Lakini polepole utawala ukabadilika. Simba akaanza kuwabagua wanyama wengine. Baadaye alijitawaza kuwa mfalme. Kwa sababu ya kula vizuri, alinenepa misuli, akajaa mikononi na kifuani akatuna kama jabali. Ndevu pia zikajaa zikaungana na nywele na kufunika shingo na kumwagika mgongoni na hata kifuani. Inasemekana kuwa mganga wa mbali alimshauri ale maini ya mnyama kila siku ili apate siha ya kutawala milele.

Tabia yake ilibadilika na hili likawashangaza wanyama wote. Kila siku ikawa mnyama mmoja anatoweka. Hiki kilikuwa kioja lakini ikagundulika kuwa uhai wao uliishia jikoni kwa mfalme. Hakuna familia ambayo haikupoteza mwenzao. Kwa kuwa Simba aliishi peke yake baada ya familia kutoweka katika mazingira yasiyoeleweka, habari zikaenea kuwa aliwaua. Baraka ikaingia kiwewe. Tatizo ni kuwa wanyama hawakuweza kufanya mkutano kwa sababu ya woga. Wakawa wanalalamika kwa kunong'onezana.

Sungura akajitolea kutafuta suluhisho. Alfajiri moja akaraukia kwa Simba. "Shikamoo mfalme Simba?"Akaanza. Simba bila hata kuinua kichwa akamfokea, "Unataka nini kinyangarika wewe?" Sungura kwa kuigiza sauti ya kutetemeka alimwambia kuwa alikuwa ametokea Simba aliyejiita mfalme wa wafalme. Simba aliamka mara moja na kutaka apelekwe aliko laghai huyo lau sivyo, angemminya sungura na kutoa ini lake.

Sungura akamwongoza Simba kidindia hadi kwenye jabali. Wanyama waliojaa hofu waliwafuata kwa mbali. Huku akionyesha chini kwenye maji sungura alimwambia Simba, "Unamwona? Unaona anavyovimba kwa kiburi na hasira?" Mwanzoni Simba hakuona kitu lakini polepole akaanzia kuona sura ya kitu majini. Akathibitisha kuwa kweli. Bila kujua kuwa kilikuwa kivuli chake aliruka kumshambulia na hatimaye kufa majini. Sungura alibebwa juujuu na kutawazwa kuwa mfalme mpya wa Baraka. Hapo wanyama wakaishi tena raha mustarehe.

31. Kulingana na aya ya kwanza
A. nchi ya Baraka ilishuhudia hali nzuri ya anga na kujitosheleza kichakula
B. kuwaka kwa jua na kunyesha mvua kulisababisha furaha isiyo kifani
C. uongozi bora wa nchi ya Baraka ulileta ufanisi usio na kifani
D. wanyama nchini Baraka hawakujua kuwa nchi huhitaji kuwa na kiongozi.

32. Hali ya kutoelewana ilizuka wanabaraka
A. walipovamiwa na njaa na magonjwa
B. kutokana na ukosefu wa kiongozi
C. walipoanza kuenda malishoni na visimani
D. idadi ilipoongezeka wakang'ang'ania rasilimali.

33. Wazee walifanya kikao ili
A. kumchagua kiongozi wa nchi ya Baraka
B. kutafuta suluhu kwa mzozo uliokuwepo
C. kufahamishana kuhusu maovu yaliyokuwepo
D. kutafuta mbinu za kupunguza idadi yao.

34. Wanyama waliofika mkutanoni
A. walimpendekeza Nyani awe kiongozi wa Baraka
B. walikaa kwenye matawi ya miti hapo karibu
C. walihofia kuwa wangeangamizwa na wenzao
D. walikuwa wa umri tofauti na jinsia zote.

35. Ni kauli gani hailingani na maelezo ya kifungu hiki?
A. Nyani alitafuta mbinu nzuri kuwasiliana na hadhira yake.
B. Wanyama walimtawaza Simba kuwa mfalme wao.
C. Wanyama waligundua umuhimu wa kuwa na mtawala.
D. Simba alikuwa kiongozi mwadilifu pale mwanzoni.

36. Maumbile ya Simba yalibadilika
A. kutokana na ulaji wake
B. kwa sababu ya ukatili
C. wanyama walipomshauri ale maini
D. kwa furaha ya kuchaguliwa.

37. Familia ziliwapoteza wapendwa wao kwa njia ipi?
A. Waliangamizwa na mfalme wao.
B. Haijulikani kwenye kifungu.
C. Waliumizwa na wenzao kwenye mizozo.
D. Waliliwa na jamaa wa Simba.

38. "Unataka nini kinyangarika wewe?" Maneno haya yanaonyesha kuwa Simba
A. hamfahamu Sungura vizuri
B. anakasirika kwa kuingiliwa asubuhi
C. na Sungura ni mahasimu wa jadi
D. ni kiongozi mwenye dharau.

39. Neno '**rabsha**' kama lilivyotumika lina maana sawa na
A. uhalifu
B. ghasia
C. kiwewe
D. ghadhabu.

40. Funzo la kifungu hiki ni kuwa
A. akili nyingi huondoa maarifa
B. ongezeko la idadi ni chanzo cha maovu
C. dhalimu hawezi kutamalaki milele
D. nchi isiyo na kiongozi hujiangamiza kabisa.

Uvumbuzi wa simutamba ni uvumbuzi ambao tunaweza kusema kuwa ni mkubwa sana katika karne hii baada ya uvumbuzi mwingine kama wa magari na runinga. Vifaa hivi vyote hutumika katika mawasiliano.

Simutamba ni suluhisho kwa matatizo mengi ambayo waja walikuwa wakikumbana nayo. Zinatuwezesha kuwasilisha mambo muhimu kwa njia ya haraka. Hebu fikiria kuna ambaye aushi yake imo hatarini lakini inakubidi upige foleni ili uweze kupiga simu. Siku hizi mambo kama hayo yamewekwa katika buku la sahau. Kutokana na uvumbuzi wa rununu, ujumbe wa haraka huweza kuwasilishwa moja kwa moja. Kabla ya uvumbuzi wa rununu au simutamba maisha ya watu yangepotea kutokana na kukosekana kwa mawasiliano bora.

Simu hii ni suluhisho kwa wale wanaoishi mashambani ambako simu za wakati huo kawaida hazikuweko. Uvumbuzi huo umempa kila insi fursa ya kuwasiliana na yeyote si nchini tu bali hata katika nchi nyingine.

Huwezi kukosa kupokea ujumbe wowote eti kwa sababu ulikuwa mahali fulani. Hivi vidumbwasha huwekwa hata vikapuni unapoenda shambani! Siku hizi uandishi wa barua ni nadra sana kwa sababu ujumbe unaweza kuwasilishwa kwa kutumia simutamba. Rununu inatupa fursa ya kutuma ujumbe kwa ada ndogo sana na ujumbe hufika wakati huo.

Rununu pia hutumika kama kifaa cha kujiburudisha. Aina za rununu zina michezo ya aina mbalimbali ambayo unaweza kucheza wakati wowote ule. Isitoshe, unaweza kupata ujumbe kupitia njia ya mtandao kupitia rununu ambazo zimetandawaziwa kutoa huduma hiyo. Rununu pia zina tarakilishi ndogo ambazo hurahishishisha mawasiliano kwa njia ya mtandao.

Baadhi ya simu hizi zina kamera. Mtu anaweza kupiga picha na kuhifadhi ili aweze kuitazama wakati wowote. Panapokuwa na kumbukumbu muhimu ambazo zinafaa kurejelewa kila mara, si lazima mtu aweke kwenye vitabu vya picha.

Licha ya hayo, simu hizi zina shajara mahsusi za kukumbusha iwapo unahitajika kuwa mahali popote na kile ambacho unahitajika kufanya. Heko kwa uvumbuzi huu kwa sababu suala la kusahau kuhudhuria mikutano halipo tena.

Hata hivyo, simu hizi huchukiza wakati mwingine. Hebu tuchukulie mfano wa mwenyekiti ambaye alikuwa akiongoza mkutano kisha akapokea simu. Labda alikuwa akiingojea simu hiyo na alifikiria kwamba angepigiwa kabla ya mkutano kuanza. Huenda ikawa simu yenyewe ni ya dharura kwa hivyo hatakuwa na jingine ila kuipokea. Je, na hao wengine waliokuwa mkutanoni wafanye nini? Wataachwa tu katika hali ya taharuki.

Nchi mbalimbali zimeanza kubuni sheria za kuzingatiwa katika matumizi ya rununu. Kuna sehemu mbalimbali ambazo mtu anahitajika azime simu. Kwa mfano, hospitalini, kwenye benki, kanisani na hata vituo vya mafuta ya petroli. **Ingawa kuna mabaya yanayoletwa na matumizi ya simutamba, zimefanya tupige hatua katika sekta mbalimbali.** Tuzielewe simutamba na tuzitumie kwa makini.

**41.** Chagua jibu sahihi kulingana na ufahamu.
A. Simutamba ndio uvumbuzi wa pekee katika karne hii.
B. Hakuna kifaa bora kuliko simutamba maishani.
C. Uvumbuzi wa simutamba umepiku uvumbuzi wa vyombo vya awali.
D. Vyombo vyote vilivyovumbuliwa katika karne hii ni vya mawasiliano.

**42.** Simu hizi hazitumiki
A. kuzuia msongamano
B. kuwasilisha ujumbe
C. kupeleka nakala za barua
D. wakati wa dharura.

**43.** Kulingana na aya ya pili
A. simu hizi zimechangia kuyaokoa maisha
B. watu walipiga foleni kuwasiliana kwa rununuu
C. magonjwa yametibiwa kwa njia ya simu
D. simutamba imetumika kwa muda mrefu kuwasiliana.

**44.** Neno lipi halifai kwenye orodha hii?
A. Simutamba
B. Tarakilishi
C. Rununu
D. Rukono.

**45.** Chagua kauli sahihi kuhusu mashambani.
A. Simutamba hazitumiki huko.
B. Mawasiliano ni bora kuliko mjini.
C. Ni vigumu kuwasiliana ukiwa huko.
D. Simu za awali zilikuwa nadra uko.

**46.** Si sahihi kusema kuwa
A. simu za rununu hubebeka kwa urahisi
B. mawasiliano kupitia rununu ni nafuu
C. rununu imechangia kuwaunganisha watu
D. watu hawajui kuandika barua sasa.

**47.** Yapi si matumizi ya rununu?
A. Kuchapisha maandishi kupata nakala.
B. Kifaa cha kujiburudisha
C. Kuhifadhi kumbukumbu muhimu.
D. Mawasiliano ya mtandaoni.

**48.** Mwandishi anasema nini katika aya ya sita?
A. Mikutano mingi huahirishwa kwa sababu ya rununu.
B. Kungojea simu nyingi hufanya mikutano kuvunjwa.
C. Matumizi ya rununu yanaweza kutatiza shughuli muhimu.
D. Watu mkutanoni hushangaa wakimwona mwenzao na simu.

**49.** Kwa nini nchi zimebuni sheria kuhusu matumizi ya rununu?
A. Watu bado hawajajua matumizi yafaayo ya simu.
B. Ili kukwepa athari zinazotokana na matumizi yake.
C. Simu hizi zimeongezeka kiasi cha kuleta madhara.
D. Mikasa mingi tunayoshuhudia inasababishwa na rununu.

**50.** Ni methali gani inayolingana na ujumbe uliopigiwa kistari kwenye aya ya mwisho?
A. Heri nusu shari kuliko shari kamili.
B. Baniani mbaya kiatu chake dawa.
C. Hakuna masika yasiyokuwa na mbu.
D. Ukitaka mawaridi vumulia miba.

***TANBIHI:*** ***Ili kudurusu kwa kina katika somo la Kiswahili, jipatie nakala ya 'KICHOCHEO CHA KISWAHILI' kutoka Signal Publishers. Kinapatikana katika maduka ya vitabu kote nchini.***